

# Chanjo dhidi ya virusi vya korona

## – Chanjo ya COVID-19 ya AstraZeneca (AstraZeneca)

---

### Maelezo kwa watu ambao wamepewa chanjo hii

Virusi vipya vya korona husababisha maambukizo ya njia ya kupumua. Watu wengi hawaonyeshi dalili zozote, au huwa na dalili ndogo, lakini wengine wanaweza kuugua sana. Watu wazee, na wale ambao tayari wameugua magonjwa mengine awali wako katika hatari kubwa ya kuugua sana au hata kufariki. Lengo la chanjo ya virusi vya korona ni kulinda maisha na afya.

### Nani wanapaswa kupewa chanjo hii ya virusi vya korona?

Watu ambao wanapendekezwa kupokea chanjo hii kupitia mpango wa kitaifa wa chanjo watapewa chanjo hii wakati ni zamu yao katika foleni ya kipaumbele.

Chanjo hii hailipishwi na ni ya hiari. Itapeanwa kwa watu wanaoishi nchini Norwe.

### Ninawezaje kupata chanjo hii?

Tembelea tovuti ya manispa ya yako upate maelezo kuhusu watu wanaopewa chanjo, jinsi chanjo inavyopangwa na wakati inatolewa.

### Chanjo hii inatolewa vipi?

Chanjo hii inadungwa kwenye sehemu ya juu ya mkono. Utapokea dozi mbili za chanjo, ya pili ikiwa wiki 9-12 baada ya chajo ya kwanza. Ni muhimu upokee dozi ya pili wakati uliopangiwa. Kabla ya kupokea chanjo, utaulizwa kama unahisi vizuri na kama umeathiriwa kwa vyovyote na chanjo zingine ulizopokea. Kumbuka kusema ikiwa una mzio wowote, ukiwa mjamzito, ikiwa unatumia dawa au una matatizo mengine ya kiafya. Ni kawaida kuchelewesha chanjo ikiwa mtu anaugua ugonjwa mkali na ana halijoto ya zaidi ya 38°C. Baada ya kupokea chanjo, utaombwa usubiri kwa dakika 20.

### Chanjo hii inafanya kazi vipi?

Chanjo hutumia virusi visivyo na makali (virusi butu) ambavyo husaidia kusafirisha kichocheo cha ncha za virusi vya korona mwilini. Mwili huunda nakala za ncha hizi ambazo mfumo wa kingamwili unaweza kutumia kufanya mazoezi. Kwa njia hii, mfumo wa kingamwili hujifunza kutambua ncha za virusi vya korona na unaweza kukinga mwili ikiwa utaambukizwa virusi.

Virusi vinavyosafirisha ncha haviwezi kuongezeka mwilini na huvunjika haraka. Chanjo haiwezi kusababisha ugonjwa wa virusi vya korona au magonjwa mengine yoyote ya kuambukiza. Chanjo ya virusi vya korona huzuia magonjwa. Haiwezi kutibu ugonjwa uliopo.

Njia hii ya kutengeneza chanjo tayari imetumika katika chanjo za Ebola.

### Chanjo hii inafanya kazi kwa kiwango gani?

Chanjo hii inalinda dhidi ya magonjwa yanayosababishwa na virusi vipya vya korona. Wiki mbili baada ya dozi ya pili, wastani wa 60% ya watu waliopewa chanjo katika tafiti

walibainika kulindwa dhidi ya ugonjwa wa COVID-19. Hata hivyo, kinga ilibainika kuwa imara zaidi ikiwa dozi ya pili ilitolewa baada ya wiki 9 au zaidi. Tafiti zinaonyesha kuwa chanjo pia hukinga dhidi ya ugonjwa mkali wa COVID-19 ambao unamhitaji mgonjwa kutibiwa hospitalini. Bado hatujajua kinga itadumu muda gani. Ikiwa kinga itapungua baada ya muda, huenda dozi nyongeza zihitajike. Kwa kuwa chanjo inazuia magonjwa, pia itazuia maambukizi, lakini bado hatujajua ni kwa kiwango gani. Kwa hivyo, ni muhimu kuendelea kufuata ushauri uliopo wa kudhibiti maambukizo.

## **Athari**

Kwa mujibu wa tafiti ambazo zimefanywa, tunafahamu vizuri athari zinazotokea mara nyingi au chache katika watu ambao wamechanjwa. Hatuwezi kutoa hakikisho kuwa hakuna athari adimu au athari ambazo huonekana tu muda mrefu baada ya chanjo. Athari nyingi zilitokea katika siku chache za kwanza baada ya chanjo, na zilikwisha ndani ya siku chache:

- Zaidi ya nusu ya watu waliochanjwa walihisi maumivu mahali ambapo walidungwa sindano.
- Athari nyingine zinazotokea mara nyingi ni kuhisi kuugua, uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli na viungo, baridi, kichefichefu na homa.
- Athari huwa dhaifu na hutokea mara chache zaidi baada ya dozi ya 2.

Katika hali nyingi, athari mbaya zilikuwa za kiwango kidogo au wastani. Chini ya 5% ya watu walikabiliwa na athari kali ambazo hazikuwa hatari, lakini ziliathiri maisha yao ya kila siku kwa siku chache ambazo athari hizi zilizodumu.

## **Nitafanya nini nikikabiliwa na madhara?**

Ukikabiliwa na dalili kali, zisizotarajiwa au zinazodumu muda mrefu ambazo unafikiri huenda zinasababishwa na chanjo, wasiliana na daktari wako au mhudumu mwingine wa afya ili kupimwe na kushauriwa. Wahudumu wa afya wana jukumu la kuripoti athari zozote mbaya au zisizotarajiwa ambazo wanashuku zinatokana na chanjo. Unaweza pia kutuma arifa mwenyewe kupitia [helsenorge.no](https://helsenorge.no).

## **Udhibitaji chini ya masharti**

Chanjo hii ya virusi vya korona imejaribiwa katika tafiti kubwa ambapo maelfu ya watu walipokea chanjo hii. Tafiti zilifanywa kwa njia sawa na tafiti za chanjo zingine, lakini kipindi cha ufuatili ni kifupi zaidi. Mamlaka za udhibiti wa dawa wametoa wameidhinisha chanjo hii chini ya masharti. Hii inamaanisha kuwa kuna data ya kutosha kuthibitisha kuwa manufaa ya chanjo yanazidi hatari zake, lakini kwamba mtengenezaji wa chanjo sharti aendelee na tafiti na kuendelea kutoa data kwa mamlaka ya udhibiti wa dawa wakati data hii imepatikana.

## **Nimepewa chanjo gani?**

Unapopokea chanjo ya virusi vya korona, utasajiliwa kwenye Usajili wa Chanjo ya Norwe, SYSVAK. Unaweza kupata maelezo yako katika [helsenorge.no](https://helsenorge.no).

## **Ungependa kupata maelezo zaidi?**

Tafadhali wasiliana na daktari wako au mhudumu mwingine wa afya au tembelea tovuti ya Taasisi ya Afya ya Umma ya Norwe kwenye [fhi.no/cvp](https://fhi.no/cvp).